Editon Consortium Journal of Kiswahili [ISSN: 2663 -9289]



Issue no: 01 | **Vol no:** 07 | **September** 2026: 111-121

Matumizi Ya Msamiati Wa Kiswahili Uliopanuliwa Maana Miongoni Mwa Wanafunzi Wa Vyuo Vikuu Katika Eneo La Magharibi Nchini Kenya

Muteshi Wilunda Joy [(1)]
Eric W. Wamalwa [(2)]
Ernest Sangai Mohochi [(3)]

(1.2.3) Kibabii University, Kenya.
Main author's email: joymuteshi@gmail.com

Article History
Received: **2026.07.17**
Accepted: **2026.08.19**
Published: **2026.09.05**

Cite this article in APA
Joy, M. W., Wamalwa, E. W., & Mohochi, E. S. (2026). Matumizi ya msamiati wa Kiswahili uliopanuliwa maana miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu katika eneo la Magharibi nchini Kenya. *Editon consortium journal of Kiswahili, 7*(1), 111-121. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v7i1.764

Ikisiri
Utafiti huu ulilenga kuchunguza matumizi ya msamiati wa Kiswahili uliopanuliwa maana miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Ulilenga kuonesha jinsi upanuzi wa maana unavyojitokeza katika maongezi yao. Wanafunzi wa vyuo vikuu wameonekana huwa na mazoea ya kutumia upanuzi wa maana. Tulichunguza msamiati wa Kiswahili ambao umepata maana mpya na kuwezesha mawasiliano yao. Uchunguzi uliozaa makala haya ulifanyika katika eneo la magharibi nchini Kenya. Uchunguzi uliongozwa na nadharia ya Semantiki Tambuzi iliyoasisiwa na Rosch (1977). Walengwa walikuwa wanafunzi wote wanaosoma somo la Kiswahili katika vyuo vikuu katika eneo la magharibi mwa Kenya. Washiriki 320 waliteuliwa kinasibu ili kuhusishwa katika utafiti. Data ilikusanywa kwa njia ya hojaji na mahojiano. Vifaa vya utafiti huu vilikuwa mwongozo wa mahojiano na hojaji. Data hii ilichanganuliwa kwa njia ya kimaelezo iliwasilishwa katika majedwali na maelezo.. Utafiti huu ulitumia usampulishaji wa kinasibu. Vyuo vikuu vitatu vilivyoteuliwa kinasibu vilihusishwa katika utafiti huu. Kupitia mahojiano na hojaji, ilibainika kwamba wanafunzi wa vyuo vikuu walitumia sana msamiati uliopanuliwa maana. Matokeo yalionesha kwamba baadhi ya msamiati wa Kiswahili umepata maana mpya ambayo inatumiwa katika mwasiliano. Mojawapo ya dhima ya upanuzi wa maana ni kuficha usiri wa wanafunzi. Pili, upanuzi wa maana ni jambo lisiloweza kuhepukika na hutokea kila uchao katika mawasiliano ya kila siku. Aidha, utafiti utachangia data muhimu katika eneo la kitaaluma itakayokuwa marejeleo kwa watafiti wa baadaye. Matokeo yalifafanua sababu zinazopelekea kuwepo kwa upanuzi wa maana.Hivyo makala haya yanapendekeza maana mpya iliyoongezwa katika msamiati huo ijumuishwe kwenye kamusi.

Maneno Muhimu: Mawasiliano, Semantiki Tambuzi, msamiati wa Kiswahili, upanuzi wa maana, wanafunzi wa vyuo vikuu.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

UTANGULIZI

Wataalam mbalimbali wameeleza dhana ya upanuzi wa maana. Upanuzi wa maana ni hali ambapo neno linalokuwa na maana maalumu huanza kutumiwa kwa maana pana zaidi au mpya. Saeed (2003) anaeleza kuwa, upanuzi wa maana hutokea wakati matumizi mapya ya neno yanapoenea katika jamii na kuanza kukubalika kama sehemu ya msamiati wa kawaida. Wanafunzi wa vyuo vikuu hutumia msamiati uliopanuliwa maana katika mazingira yao. Kutokana na hali hiyo, msamiati wa Kiswahili hupitia mabadiliko ya kimaana ambapo neno moja linaweza kupata matumizi mapana zaidi kuliko hapo awali. Hali hii imechangia katika utafiti huu kwani tumechunguza jinsi wanafunzi wanavyotumia msamiati huo na jinsi maana inavyojitokeza katika mazumgumzo yao.

Traugott & Dasher (2002) wanaongeza kuwa, mabadiliko haya ya maana hutokana na matumizi ya kila siku ya lugha ambapo wazungumzaji hujaribu kuleta ubunifu, kuficha ujumbe au kuendana na mazingira mapya ya kijamii. Kwa mfano, neno ambalo awali lilikuwa na maana hasi linaweza kupanuliwa na kupata maana chanya kulingana na muktadha wa matumizi. Wanafunzi wamefanikisha kuwepo kwa matumizi haya hivyo kupelekea utafiti wetu katika sehemu hii. Kwa mujibu wa watafiti hawa, upanuzi wa maana hutokea pale ambapo maana ya neno huenea kutoka matumizi mahsusi hadi matumizi ya jumla zaidi. Jamii inapobadilika, watumiaji wa lugha hulazimika kutumia maneno yaliyopo kuelezea hali mpya ya maisha.

Vijana ni miongoni mwa wanajamii walio wepesi katika mchakato wa upanuzi wa maana. Hali hii inajitokeza pia katika vyuo vikuu nchini Kenya na kwingineko. Makala haya yamelimulika hili kwa kujikita katika eneo la Magharibi, nchini Kenya. Makala haya yamegawika katika sehemu ya utangulizi imefuatiwa na uhakiki wa maandishi. Vilevile, kuna msingi wa nadharia, mbinu za utafiti, matokeo na mjadala, mapendekezo ya tafiti za baadaye, maadili katika utafiti na kisha marejeleo.

MAPITIO YA MAANDISHI

Mabadiliko ni jambo ambalo hutokea kwa lugha zote zinazotumiwa.Kupitia katika uhakiki wa maandishi ilionekana kwamba hakukuwa na tafiti zilizoshughulikia upanuzi wa maana. Tafiti chache pia zilitumia nadharia ya Semantiki Tambuzi. Rajab (2015) alitafitia tathmini ya mabadiliko ya maana ya msamiati wa Kiswahili katika muktadha wa kisiasa. Utafiti wake ulijikita katika muktadha wa siasa. Nadharia zilizotumika katika utafiti wake zilikuwa nadharia kidhi ya mawasiliano, nadharia ya ubadilikaji na nadharia ya mwenendo wa mabadiliko. Mtafiti alichambua data iliyokusanywa nyanjani kwa kuongozwa na malengo ya utafiti wake. Data ya utafiti ilichanganuliwa kwa kutumia asilimia ili kuonesha idadi ya msamiati uliobadili maana. Kamusi ya BAKITA (2015) na Kamusi ya Karne ya 21 (2013) zilitumika ili kupata maana ya msamiati. Utafiti wetu pia ulitumia kamusi ili kuorodhesha msamiati ambao maana yake imepanuliwa. Vilevile tulitumia mbinu hii ya uchanganuzi tulipoorodhesha maana asili na maana iliyopanuliwa. Data pia ilichanganuliwa kupitia mwelekeo wa kisemantiki. Utafiti huu ulitupa mwanga wa mbinu za mabadiliko ya maana na uchambuzi wa msamiati uliokusanywa nyanjani.

Goyvaerts (1975) anadai kwamba, kuna ushahidi unaodhibitisha kuwepo kwa mabadiliko ya lugha. Ushahidi huu unajitokeza kupitia othografia na maandishi ya kale. Maandishi ya kisanaa pia yanaonesha mabadiliko ya lugha. Maandishi haya yamedumu muda mrefu bila kutoweka. Kazi za wanaisimu wa zamani pia zinadhibitisha kuwepo kwa mabadiliko katika lugha. Aidha, mtagusano wa jamii mbalimbali pia ni ushahidi kuwa mabadiliko yanatokea katika lugha. Kupitia kwa usomaji wa kazi za wanaisimu wa zamani, tuligundua kwamba upanuzi si jambo geni katika lugha zote. Maandishi hayo yalitusaidia katika uchanganuzi wa data tuliyolusanya nyanjani.

Odawo (2015) alitafitia uhamishaji wa maana katika mchezo wa kandanda. Lengo la utafiti wake lilikuwa kutambua mbinu za mawasiliano zinazotumiwa na watangazaji wa mchezo wa kandanda na kubainisha msimbo wa maana inayoibuliwa kutokana na matumizi ya lugha. Utafiti huu ulingozwa na Sarufi Amilifu Mfumo iliyoelezea tukio la kijamii, lugha iliundwa kwa minajili ya kuwezesha mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali. Data ilichanganuliwa ikizingatia maswali na malengo ya utafiti na kuwasilishwa kupitia njia ya maelezo. Mbinu hii pia ilitufaa katika uchanganuzi wetu wa data. Mbinu zilizobainishwa katika utangazaji wa mchezo wa kandanda zilikuwa kama uchanganyaji msimbo, takriri, tashhisi, semi na methali.

Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Semantiki Tambuzi. Nadharia hii iliasisiwa na Rosch (1977). Nadharia hii imetokana na mchipuko wa sayansi tambuzi

na fikira za awali za mwanafalsafa Gesalt pamoja na tafiti zilizohusu jinsi binadamu wanavyoanisha vitu. Katika Semantiki tambuzi, maana ya usemi hulinganishwa na mifumo ya kiakili. Iliboreshwa mwaka wa 1977 kama sehemu ya isimu tambuzi ambayo ilipinga madai kuwa semantiki ilikuja baada ya sintaksia ilivyodaiwa. Ni mojawapo ya nadharia pana ya isimu tambuzi.

Rosch (1977) alizidi kusema kuwa, mifano ya makundi hutegemea sana mchakato wa saikolojia ambao huweza kupimika. Misingi ya nadharia hii ni kuwa maana ya maelezo yoyote ni za bongoni na huiona lugha kama sehemu ya muundo tambuzi bali si dhana inayojisimamia. Muundo wa kisemantiki katika nadharia hii hujikita katika utambuzi na hivyo maana huwa imo bongoni mwa msemaji wa lugha. Maneno mara nyingi huwa hayawakilishi yale yanayoonekana kwenye makamusi bali huwa kama mlango wa kufikia hifadhi kubwa ya maarifa kuhusiana na dhana fulani.

Mhimili wa kwanza wa nadharia hii ni kuwa lugha ni sehemu ya utambuzi kwa ujumla. Mhimili huu ulitumiwa katika uchambuzi wa ujitokezaji wa maana iliyopanuliwa. Lugha hushughulikia hisia za kisaikolojia. Saikolojia hudadisi akili na mienendo ya binadamu na hivyo pana uhusiano wake na lugha. Hadumond (1996) anasema kuwa kuna kanuni ambazo zinamtawala mtu katika kuchagua lini na kwa nini ataamua kusema na mtu fulani huku akitumia mtindo tofauti kila anapobadilisha muktadha wa mazungumzo. Katika mawasiliano ya kila siku, binadamu hubadili maneno au msamiati kwa kutegemea muktadha. Wanafunzi hali kadhalika hubadili msamiati ikitegemea na mahali walipo na kile wanachorejelea ili waelewane kwa njia ya kipekee. Mhimili huu ulitufaa tulipokuwa tukichanganua mbinu ambazo msamiati umetumiwa katika mabadiliko yao. Mbinu ya sitiari ilionekana kutumia saikolojia ya washiriki katika upanuzi huo wa maana. Hisia za kisaikolijia zilibainika kupitia upanuzi wa maana hivyo mhimili huu kuwa faafu.

Pili, nadharia hii huongozwa na mhimili kuwa kiini cha lugha ni kuwasilisha maana na ni sharti lugha yoyote inayotumiwa na mwanadamu iwe na uwezo wa kukamilisha mawasiliano. Pasi na hilo, basi lugha huenda ikakosa umuhimu. Utafiti huu ulijikita mno katika sehemu ya maana. Mhimili huu ulitumika katika kuangazia maana ambayo msamiati uliopanuliwa. Ilibainika kwamba msamiati huo uliopanuliwa ulipata maana inayoeleweka na wazungumzaji hivyo kiini cha lugha kuafikiwa. Mawasiliano yaliafikiwa na ule upanuzi wa maana.

Tatu, maana huwa imejikita katika maumbile ya binadamu yakiwa msingi wa kufasiri dhana katika ulimwengu wake. Lemmens et al. (2017) wanaeleza kuwa, maumbile ya binadamu humjengea msingi wa kutambua dhana mbalimbali katika mazingira yake; wanaisimu wakiita picha au taswira. Hivyo binadamu husimbua maana kwa jinsi anavyofasiri ulimwengu wake. Wanafunzi hufasiri maana katika ulimwengu wao wa shuleni na mazingira hayo. Taswira ya binadamu huchangia wakati ambapo wanapanua maana ya msamiati wao. Maana hiyo kwa mara nyingi huenda kufanana na maana asili ya msamiati husika. Kupitia mhimili huu, taswira ya wanafunzi katika upanuzi uliafikiwa. Taswira ya mwonjo, mguso na umbo zilionekana katika upanuzi wa maana miongoni mwao na kuchanganuliwa katika utafiti huu.

Nne, maarifa ya kiutambuzi huwa katika kategoria zenye mzunguko na uzito wa maana hufifia kutoka kwa kiini maana. Greens (2006) anaeleza kuwa leksia ni chombo kinachotumika na wazungumzaji katika kuafikia maarifa yaliyopo katika hifadhi ya maarifa katika utambuzi. Lugha hubadilika na maana yake huweza kufifia kutoka kwa kiini maana. Kwa mara nyingi katika upanuzi wa maana, ile maana iliyoongezewa inaweza kufifia kutoka kwa kiini maana. Maana iliyopanuliwa huwa haina uzito mwingi ukilinganisha na maana asili. Tofauti kati ya maana zile huwa haikui kubwa sana. Maana katika msamiati ilionekana kufifia kutoka kwa maana yake ya asili. Maana ilichanganuliwa na kugundua kwamba maana iliyopanuliwa inabeba maarifa ya kiutambuzi. Hii ilionekana tulipochambua maana ya awali na maana asili na kupata ulinganisho huo.

MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia mbinu za mahojiano na hojaji. Maswali yaliulizwa ili mtafiti apate ufahamu wa jinsi wanafunzi wa vyuo vikuu wanavyopanua maana ya msamiati. Mahojiano yaliandaliwa na kutumiwa kusanya taarifa za kina zaidi.Wanafunzi hao walikuwa makundi manne ya wanafunzi ishirini na watano wa kila mwaka kwa kuzingatia vigezo vya chuo, jinsia, somo na lugha ya kwanza.Wanafunzi 300 walipewa hojaji kisha wakazijaza. Maswali yaliyotumika katika utafiti hojaji yalikuwa wazi na funge. Hii ilituwezesha kupata ujumbe wote ambao tulikusudia kukusanya kutoka nyanjani.

Uchanganuzi wa data ulikuwa wa kimaelezo na kitakwimu. Majedwali yalitumika kueleza data hiyo. Sampuli iliyotumiwa katika utafiti huu iliwashirikisha wanafunzi wa vyuo vikuu kuanzia mwaka wa kwanza hadi nne. Wanafunzi mia tatu ishirini (320) utoka katika vyuo vikuu vitatu walishirikishwa. Hojaji mia tatu zilitumiwa kukusanya data na wanafunzi ishirini walihojiwa.Uteuzi wa sampuli ya wanafunzi ulitekelezwa kwa kuzingatia kigezo cha Saunders, Thornill & Lewis (2009) walioeleza kwamba, kuna idadi ndogo kabisa ya sampuli inayohitajika kutoka idadi tofauti ya wigo na ambayo huwa na kiwango cha utegemevu cha asilimia 95 na kiwango cha makosa wa kuongeza au kutoa asilimia 5. Hali hii iliwezekana kwa kupata idadi kamili ya watafitiwa wote kutoka wigo nzima.

Vyuo vikuu vya umma vilivyoshirikishwa viliteuliwa kinasibu. Majina ya vyuo vikuu tisa vinavyopatikana eneo la magharibi yaliandikwa na kutiwa kwenye boksi kisha mtafiti akaokota karatasi tatu kati yazo. Wanafunzi hawa walichaguliwa kwa kutumia usampulishaji tabakishi na wa kinasibu.Utafiti ulipata kibali kutoka kwa Bodi ya maadili ya Chuo Kikuu cha Kibabii. Washiriki walitia sahihi fomu za radhi kabla ya utafiti kufanyika.

MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii imezingatia uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo kuhusu upanuzi wa maana ya msamiati wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Msamiati huu ulikusanywa katika vyuo vikuu vitatu. Chuo kikuu Cha Kibabii, Maseno na Chuo kikuu cha Masinde Muliro.

Tulipata makundi matatu ya aina za maneno ambayo ni: nomino, vivumishi na vitenzi. Katika vitenzi, tulichanganua kulingana na mianzo yake kialfabeti. Vivumishi vilichanganuliwa bila kugawanywa kwenye makundi. Uchanganuzi wa utafiti huu pia ulionesha kwamba upanuzi wa maana huchukua mielekeo tofauti tofauti. Mielekeo hii ni kama vile ufinyizi wa maana, udhalilikaji wa maana, sinedochi, metonimi na uimarikaji wa maana.

Nomino Zilizopanuliwa Maana

Kihoro na wenzake (2003) wanafasili nomino kama jina linalotaja kitu, kiumbe hai au dhana. Wataalam hawa wanazidi kusema kuwa nomino zimegawanywa katika sehemu mbili nazo ni nomino mahususi na nomino za kawaida.

Maana ya asili ilipatikana katika kamusi ya karne ya (21) na BAKITA (2015) na maana mpya ilivyojitokeza katika hojaji au jinsi wanafunzi wanavyotumia msamiati husika. Katika Kiswahili cha sasa, hasa miongoni mwa vijana wa vyuo vikuu, maneno kama *balaa*, *mzinga*, *keki* na *jaba* yamepata maana mpya zinazotofautiana na maana zake za awali. Katika kundi hili, tulichanganua nomino zilizopanuliwa na kurejelea mapenzi, sehemu za mwili na mambo mengine ya kawaida.

Utafiti huu ulionesha kwamba, baadhi ya nomino zilipata maana inayohusiana na mapenzi au hali ya kushiriki mapenzi. Baadhi ya nomino hizi ni kama vile "mechi" ambayo imepata maana mpya kulingana na wanafunzi wa vyuo vikuu. Kulingana na Kamusi ya Kiswahili toleo la tatu (2014) neno mechi ni nomino ya kawaida inayomaanisha mashindano baina ya timu mbili.

Mfano 1*: Nitatazama **mechi** ya Gor mahia na Asenali.*

Sentensi hii inamaanisha kuwa mzungumzaji atatazama mchuano wa mpira kati ya Arsenal na Gor Mahia. Maana ya pili ya nomino hii ni kupatana kijamii au mahusiano. Ni kitu au watu wanaopatana tabia na mawazo.

Mfano 2:*Marafiki hao ni **mechi** nzuri ajabu.*

Nomino hii inaweza kumaanisha mchezo wa mashindano ulinganifu au upatanifu kulingana na muktadha. Wanafunzi wa vyuo vikuu wamepanua maana yake na kuifanya kurejelea hali ya kushiriki ngono kati ya wapenzi wawili. Maana ya msamiati huu uliopanuliwa inaelekea kufanana na ile maana ya timu mbili. Mechi ni msamiati unaotumiwa sana na wanafunzi hawa ili kuficha tabia ambazo ni za aibu kuzungumziwa na watu hadharani. Jinsi inavyotumiwa.

*Mfano 3: Niliitiwa **mechi** jana usiku.*

Nomino mbao ina maana ya sehemu ya mti au gogo iliyopanuliwa na kutengeneza vitu kama kabati, chombo chenye rangi ya kijani na nyeusi kinachochomelewa ukutani na kuandika kwa chaki. Nomino hii imepanuliwa maana na kumaanisha hali ya mtu wa asili ya kiume kuwa na mwasho au ari ya kushiriki ngono. Hali hii huonekana kama sehemu ya mti hivyo ulinganisho huu wa kisitiari. Nomino Kiswahili vilevile imepokea maana mpya. Maana asili ya nomino hii ya pekee ni lugha ya kibantu ambayo huzungumzwa Afrika Mashariki ikiwa na wasemaji kadri milioni mia mbili wanaoitumia kama

lugha yao ya kwanza na ya pili. Hii ni lugha inayoenziwa na watu wengi na ni lugha ya taifa nchini Kenya.Halikadhalika kutokana na upanuzi wa maana, jina hili Kiswahili limepata maana ya jambo gumu linalohitaji kufikiria sana ndiposa litatulike. Kwa mara nyingi watu wengi huona lugha hii kuwa ngumu na hivyo wanafunzi wakarejelea hivi. Maana hii imefifia kutoka kwa kiini maana.

*Mfano 4: Hiyo exam ilikuwa **Kiswahili** kweli.*

Nomino uji kwa pia ni nomino ya wingi inayorejelea chakula chepesi rojorojo ambacho kinapikwa kwa kuchemsha nafaka, unga au chenga za nafaka. Uji hutumia haswa na watoto wanaoanza kula kwa mara ya kwanza. Neno uji kwa mujibu wa maelezo haya inafanana na aina ya pombe ambayo huitwa "busaa" kwa lugha ya kawaida. Wanafunzi wamepanua maana ya msamiati huo na kurejelea pombe. Mtafiti aliwahoji wanafunzi ili kubaini ni nini haswa walizingatia na wakasema kuwa ni ule mfanano ndio umeleta upanuzi huo.

Mfano kimatumizi: Kamau hunywa maji kila jioni

Nomino maji ni nomino ya wingi. Nomino hizi ni zile ambazo haziwezi kuhesabika. Nomino hii ina maana ya kitu kiowevu kisicho na ladha wala rangi kinachopatikana mitoni, kwenye maziwa na mabwawa. Sentensi: Mama alinituma mtoni kuteka maji. Nomino hii imepata maana ya pombe. Maana hii inaelekea kufanana na maana ya awali kwa taswira ya mwonekano. Pombe huwa na mfanano wa maji.

Mfano 5: *Mwanahamisi anapenda kunywa **maji** sana wakati wa jioni kwenye kilabu cha Beua.*

Kupitia utafiti wetu, ilibainika wazi kwamba wanafunzi wa jinsia ya kiume walupanua maana ukilinganisha na wanafunzi wa kike. Baadhi ya wanafunzi wa kike walikiri kutokuwa na ule uzoefu wa kutumia msamiati ambao maana yake imepanuliwa. Kupitia nomino zilizopanuliwa maana, insjitokeza vyema kwamba upanuzi huo huwa si mbali sana na maana yake asili. Upanuzi umetumia maana asili kutengeneza maana mpya. Kupitia utafiti wa Rajab (2015) ilionekana kwamba katika mabadiliko ya maana, uhusiano wa maana asili a ya awali huwepo.

Jedwali 1: Nomino Zilizopanuliwa Maana

Msamiati	**Maana asili**	**Maana mpya iliyopanuliwa**
Mechi	Kandanda	Shiriki tendo la ndoa
Uwanja	Mahali pa kucheza	Kitanda
Katiba	Sheria au kanuni	Sehemu ya siri hasa ya mwanamke
Paka	Mnyama mdogo anayekula nyama, anayefugwa nyumbani kwa ulinzi dhidi ya wanyama waharibifu kama panya	Sehemu ya siri ya mwanamke
Mti	Mche/ mmea wenye shina gumu unaoota mwituni au kupandwa shambani	Sehemu ya uume wa mwanaume
Mkwaju	Mti mkubwa wa kijani kibichi unaozalisha matunda ya ukwaju yenye ladha ya kuchachuka	Sehemu ya uume ya mwanaume
Mrija	Kibomba kidogo chembamba cha kufyonza vitu majimaji	Sehemu ya utupu wa mwanaume
Uji	Chakula chepesi rojorojo ambacho kinapikwa kwa kuchemsha nafaka, unga au chenga za nafaka	Pombe
Maji	Kiowevu kisicho na rangi au ladha kinachopatikana kwenye mito, bahari au kwenye maziwa na wakati mwingine hutokana na viumbe hunywa, kupika kuogea.	Pombe
Jembe	Zana inayotengenezwa na chuma inayotumiwa kuchimba ardhi	Mtu mwenye bidii shupavu/ gwiji

Chanzo: Utafiti nyanjani (2026)

Vitenzi Vilivyopanuliwa Maana

Upanuzi wa maana umejitokeza kupitia vitenzi. Kitenzi ni neno linaloonesha tendo, hali au mchakato unaofanywa au unapotokea kwa mtenda. Massamba (2004) anaeleza kwamba kitenzi ni neno linaloonesha kitendo au hali inayohusishwa na mtenda. Katika utafiti huu, tulipata vitenzi vingi ambavyo maana yake imepanuliwa. Tuligawa vitenzi hivi huku tukizingatia herufi za mwanzo.Tulipata vitenzi vilivyoanza na herufi b,c,d,f,g,I,k,l,m,n,o,p,t,u,w na z.

Vitenzi hivi vilikuwa kama gawa.

Kitenzi gawa kina maana ya kugawanya au kutia kitu kwa watu wengi ila kila mmoja apate sehemu.

*Mfano 6: Ali**gawa** chakula kwa wageni.*

Maana iliyopanuliwa ni kushiriki mapenzi na watu wengi bila ubaguzi.

*Mfano 7: Anajulikana kwa ku**gawa** sana chuoni.*

Uhusiano kati ya maana hizi mbili umefananishwa na kuwa kugawa kitu huhusisha watu wengi, hufanyika bila kuchagua na kila anayehitaji hupata sehemu yake. Uhusiano wa kimapenzi ya mtu anayegawa huhusisha watu wengi, hufanyika bila upendeleo, mapenzi unaonekana kuwa rasilimali inayotolewa kwa wengi. Upanuzi umejitokeza kupitia njia ya sitiari. Huu umeoonesha mtazamo wa kijamii kuhusu tabia ya kimahusiano. Kuonesha msisitizo wa wingi au kutochagua na kutoa hukumu ya maelezo ya jamii isiyo ya moja kwa moja.

Gonga

Maana ya kimsingi ya gonga ni kitendo cha kupiga kwa nguvu au mgongano wa vitu viwili.

*Mfano 8: Mtoto ali**gonga** mlango.*

Hapa kuna mgongano kati ya mkono wa mtoto na mlango. Maana iliyopanuliwa ni hali ya kushiriki ngono. Gonga imetumika kama kitendo cha ngono kwani ngono inafanana na mgongano wa miili kama kugonga kitu na pia ni kitendo cha mara kwa mara na kwa nguvu.

*Mfano 9: Wali**gonga** mke wangu Fatuma.*

Kugongewa nayo ni kitendo cha mtu mwingine kushiriki ngono na mkeo au mumeo.

*Mfano 10: Nili**gongewa** bibi na rafiki yangu.*

Jedwali 2: Vitenzi Vilivyopanuliwa Maana

Msamiati	**Maana asili**	**Maana mpya iliyopanuliwa**
Gonga/ Gongewa	Kitendo cha kupiga kwa nguvu au mgongano wa vitu viwili	Ibiwa mke
Gawa	Tengeneza watu au vitu katika makundi madogo madogo Sambaza miongoni mwa idadi ya watu Tegemea jasho la mtu	Shirika mapenzi na kila mtu bila ubaguzi
Tesa	Dhalilisha mtu	Kufanya watu wakutamani
Tisha	Kutia hofu, wasiwasi	Kitu bora/ kuvutia
Toboa	Dunga na kutengeneza shimo	Faulu kufanya jambo
Tupa	Peleka au vugumiza kitu linachohitajika kwenye kikapu au shimo la taka Acha bila kutunza au kuangalia Rusha kitu kutoka ulipokwenda	Sahau mtu
Teka	Chukua kitu kiowevu kwenye maji au bakuli	Kumpenda mtu
Beba	Inua kitu	Kuwa na makalio makubwa
Choma	Teketeza kwa moto	Haribu jambo au tenda kitendo cha aibu
Chapa	Piga kwa bakora	Onekana vibaya
Okoka	Nusurika kupatwa na jambo baya Epuka jambo kwa bahati Epuka hatari za kiroho, wacha dhambi na kujisalimisha kwa Mungu	Kujiona bora kuliko wengine
Lenga	Tafuta shabaha kwa kuelekeza kitu kwa utulivu kmf bunduki pasua kitu kwa mfano gogo, muwa kwa vipande vidogo vidogo na virefu	Kumdharau au kumhepa mtu fulani
Winda	Fukuza mnyama kwa lengo la kumkamata	Tendo la kutafuta mchumba

Chanzo: Data nyanjani (2026)

Vivumishi

Vivumishi ni maneno yanayotoa taarifa ya ziada, kuelezea sifa, au kubainisha nomino au kiwakilishi katika sentensi. Kazi yake kuu ni kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu ukubwa, rangi, umbo, umiliki, au idadi ya kitu.

Katika jedwali hili, tumepata vivumishi vitatu. Kivumishi kali kimepata maana mpya ambayo inamaanisha kitu kinachovutia macho au kitu kirembo. Mbaya imepata maana mpya na kuanza kumaanisha kitu bora tofauti na maana yake ya awali ambayo ni kitu ambacho si kizuri. Kivumishi baridi vile vile kilipata maana ya kutofurahia kitu au kuwa na uoga. Kivumishi hiki kimepanuliwa maana kwa ulinganisho wa kisitiari ya hali ya baridi ambayo huenda kufanana na hali ya kuwa na uoga fulani.

Jedwali 3: Idadi ya Vivumishi

VIVUMISHI			
	Msamiati	**Maana asili**	**Maana mpya iliyopanuliwa**
1.	Kali	Enye ubapa ulionelewa na unaoweza kukata kitu kilichochongoka Enye kupenda kudhuru kmf kuuma, kukaripia Enye ladha ya pilipili iwapo mdomoni Enye kuchenyeta mwilini	Kinachovutia kwa macho Kitu kirembo
2.	Mbaya	Si nzuri	Kitu bora
3.	Baridi	Kutokuwa na joto	Kutofurahia kitu Kuwa na uoga

Chanzo: Data nyanjani (2026)

Msamiati Uliopanuliwa Kimafumbo

Baadhi ya semi zinazotumiwa ziliongezewa maana na kupata maana iliyo tofauti na jinsi zilitumiwa awali. Semi hizi za kimafumbo kwa mara nyingi hutumiwa kuficha ukweli wa jambo fulani. Jedwali hili limeorodhesha semi hizi kama zilivyokusanywa nyanjani.

Jedwali 4: Msamiati Uliopanuliwa Kimafumbo

Neno	**Maana ya awali**	**Neno jipya la kimafumbo**
Rudi soko	Enda sokoni	Tendo la kutafuta mchumba
Tupa mbao	Tendo la kutoa mbao mkononi	Poteza kitu cha muhimu
Uma nje	Kupitiza neno mahali pasipo stahili bila kulenga shabaha	Kosa kitu au jambo Kutofanikiwa
Safisha nyumba	Kufagia/ kupiga deki	Kufukuza mpenzi
Chonga kinyago	Kutengeneza sanamu	Kushiriki ngono
Panda mbegu	Kutia miche shambani	Kupachika mimba
Piga mswaki	Kusafisha meno	Kunywa pombe
Pika chai	Kupika kinywaji	Shiriki mapenzi
Cheza chini	Fanya jambo la kuchangamsha mwili au kujifurahisha ukiwa sakafuni	Hali ya kumsihi mtu asizungumzie kitu au kufanya jambo ambalo halikubaliki
Piga kelele	Kutoa sauti inayokera	Kugombana
Piga mbizi	Kuogelea majini	Chunguza jambo kiundani
Kitu kidogo	Kitu haba	Rushwa
Kuwa chini	Kuwa sakafuni au ardhini	Kosa hela
Ona giza	Kutoona mwanga	Kupata jambo gumu

Chanzo: Data nyanjani, 2026

Upanuzi wa maana hutokea pale ambapo maana hubadilika na kuwa pana kuliko ile ya asili. Hii ni pale ambapo inapata maana zaidi na ya awali. Upanuzi ulionekana kuchukua mielekeo na hizi ni baadhi ya mielekeo ya upanuzi wa maana.

Udhalilikaji wa Maana

Hii ni pale ambapo neno hubadili maana kutoka chanya hadi hasi katika matumizi yake (crystal, 1987). Msamiati huanza kuwa na maana duni na kupunguza ukubalikaji wake kwa jamii.

Aidha msamiati pindua pia umedhalilishwa maana ya awali na kuanza kumaanisha kumdhulumu mtu.

Msamiati okoka umedhalilika maana kutoka kwa jambo baya au epuka kwa bahati au kujisalimisha kwa Mungu hadi maana ya mtu anayejiona bora kuliko wengine. Hamna anayetoka kujihusisha na neno hilo kwa sababu ya udhalilikaji.

Jedwali 5: Udhalilikaji Maana

Msamiati	Maana asili	Udhalilikaji maana
Lenga	Pata shabaha	Kumdharau au kutomtambua mtu
Mechi	Mashindano baina ya timu mbili katika mchezo kama vile kandanda	Tendo la ndoa
Maji	Kitu kiowevu kinachotumiwa kupika au kuoga	Pombe

Kuimarika kwa Maana

Hii hutokea pale ambapo msamiati hubadilika maana kutoka kwa maana hasi hadi maana chanya. Wakati lugha unakua, mabadiliko haya huweza kutokea.

Katika mfano wa kwanza, neno tesa ambalo lina maana ya kumdhulumu mtu na kumpitishia shida nyingi limeimarika maana na kumaanisha kitu kuwa kirembo au kupendeza na kuvutia. Msamiati kiburi ambao unamaanisha mtu mwenye ujeuri unaimarika na kumaanisha mtu anayejiamini kwa kazi zake. Msamiati mchokozi ambao maana yake ni mtu anayemfanyia mwingine visa vya kukasirisha au kuzua ugomvi imeimarika na kumaanisha mtu mcheshi. Maana hii imetoka kwa maana hasi na kupata maana nzuri hivyo kuimarika maana (Rejelea jedwali 6).

Jedwali 6: Kuimarika Maana

Msamiati	Maana asili	Maana uliyoimarika
Tesa	Piisha kiumbe maumivu au taabu	Pendeza kwa macho
Kiburi	Hali ya mtu kujiona bora kuliko wengine	Mtu mwerevu
Umwa	Pata au hisi maumivu	Pendeza
Kali	Enye ubapa ulionolewa	Vutia
Mchokozi	Mtu anayemfanyia mwingine visa vya kukasirisha au kuzua ugomvi	Mcheshi

Utafiti (2026)

Sitiari

Lakoff na Johnson (1980) wanaeleza kwamba sitiari ni mchakato wa kuhamisha dhana kutoka kwa wanda moja na kuchopeka dhana tofauti kwa wanda jingine. Kulingana na nadharia ya Semantiki Tambuzi maana ya msamiati hauwezi kueleweka bila kuhusisha maarifa ya kiensaiklopidia ya msamiati huo. Maana mpya ya msamiati uliopanuliwa hufahamika kupitia hali ya mfanano wa msamiati huo.

Kwa mfano neno choma lina maana ya tendo la kuteketeza kitu au kuharibu kwa moto. Katika upanuzi wa maana, msamiati huu umepanuliwa na hivyo kurejelea kuharibu jambo au kutenda jambo la aibu. Kupitia kwa msamiati huu, mahusiano ya kisitiari yanaonekana kwani maana zote zinarejelea kuharibu kitu. Kupitia mbinu hii ya sitiari, kuna vikoatofauti vinavyoonekana. Mawanda haya ni kama vile,

Uhusiano wa Kiumbo na Kimaumbile

Huu ni uhusiano unaohusu umbo la kitu. Maumbile haya ndiyo msingi wa kutambua dhana katika ulimwengu wa mwanadamu. Maana ya msamiati B ni ile iliyopanuliwa na A ni ile ya awali. Umbo la A ndiyo nayopelekea kuwepo kwa maana. Kutokana na usemi wa wahojiwa, ilidhihirika kuwa nomino mpira huonekana kufanana umbo na mama aliye mjamzito hivyo ikapelekea ulinganisho huu katika kupanua maana ya msamiati huo. Maana ya msamiati B ni ile iliyopanuliwa na A ni ile ya awali. Umbo la A ndiyo nayopelekea kuwepo kwa maana. Kutokana na msamiati beba, tunaweza sema kuwa uzito wa kitu ndio unaopelekea upanuzi huo kutokea.

Leksia iva iliyo na maana ya fika upeo wa kukua imepanuliwa maana na kumaanisha mrembo mwenye sura nzuri. Maana hizi mbili zinaonekana kufanana

kulingana na maumbile ya vitu hivyo viwili. Kwa mara nyingi, Tunda lililoiva au kitu chochote kilichoiva huonekana kuvutia macho ya yeyote yule anayetazama na kuleta hali ya kutaka kuila. Odawo (2015) katika utafiti wake iligunduliwa kwamba pana semi ambazo zilitumika katika uhamishaji wa maana ya msamiati katika mchezo wa kandanda. Hali ni ile ile katika matumizi ya msamiati uliopanuliwa maana.Rejelea jedwali 7.

Jedwali 7: Uhusiano wa Kiumbo na Kimaumbile

Msamiati	**A**	**B**	**Uhusiano wa A na B**
Beba	inua kutoka ardhini	kuwa mnene kupindukia	Uzito kutoka kwa kitu
Waka	Toa nuru au mwanga	Haribu jambo au fanya kitu cha aibu	Hali ya uharibifu
Iva	Fika upeo wa kukua	Mrembo mwenye sura nzuri	Hali ya kuvutia
Paka	Mnyama anayefugwa anayependa kula panya	Utupu wa mwanamke	Maumbile
Mrija	kibomba kidogo chembamba Cha kunyunyizia vitu maji	Sehemu ya utupu wa mwanaume	Maumbile
Maji	Kitu kiowevu kisicho na ladha kinachopatikana mtoni ambacho hutumiwa kufua, kupika na kadhalika	Pombe	Maumbile
Mtoto	Mwana	Mchumba	Mwonekano wa kuvutia

Utafiti (2026)

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Hitimisho: Makala haya yamejadili jinsi upanuzi wa maana unavyojitokeza miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu katika eneo la magharibi nchini Kenya. Makala haya yameshughulikia swali kuu la utafiti huu ambalo lilinuia kueleza ujitokezaji wa upanuzi wa maana miongoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Katika uchunguzi huu, makala yameonesha kwa kutumia majedwali na kuainisha maana asili ya msamiati na maana iliyoongezeka. Makala haya yanachangia katika isimu ya Kiswahili kwani inatoa orodha ya msamiati inayopaswa kuongezwa kwenye kamusi. Pia, inadhibitisha nadharia ya Semantiki tambuzi katika muktadha wa Kiswahili.

Mapendekezo: Imependekezwa tafiti za baadaye zishughulikie upanuzi wa maana kwa watumizi wengine wa lugha wasio wanafunzi. Aidha, utafiti linganishi pia ufanywe kati ya wanafunzi wa vyuo vikuu na vijana wasio wa vyuo ili kuona kama upanuzi wa maana ni la kundi maalum au la. Pia, utafiti katika upanuzi wa maana miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili unaweza fanywa. Aidha, pana haja ya kuchunguza upanuzi wa maana katika mitandao za kijamii.

MAREJELEO

Bakita. (2015). *Kamusi kuu ya Kiswahili*. Longhorn Publishers.

Crystal, D. (1987). *The Cambridge encyclopedia of language*. Cambridge University Press.

Goyvaerts, D. L. (1975). *Present-day historical and comparative linguistics: An introductory guide to theory and method*. E. Story Scientia.

Greens, S. (2006). *Cognitive linguistics: An introduction*. Edinburgh University Press.

Hadumond, B. (1996). *Routledge dictionary of language and linguistics*. Routledge.

Kihoro, Y. M., Massamba, D. P. B., & Msanjila, Y. P. (2003). *Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu (SAMAKISA): Sekondari na vyuo*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Lemmens, M. (2017). Cognitive semantics. In N. Riemer (Ed.), *The Routledge handbook of semantics*. Routledge.

Massamba, D. B. (2004). *Kamusi ya isimu na falsafa ya lugha*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Odawo, A. M. (2015). *Uhamishaji maana katika sajili ya mchezo wa kandanda* [Tasnifu ya uzamili, Kenyatta University]. https://ir-library.ku.ac.ke/items/46bf9d5d-f579-47ea-b9ad-be287d6dcc05

Rajab, T. (2015). *Tathmini ya mabadiliko ya maana ya msamiati wa Kiswahili katika muktadha wa kisiasa: Mfano kutoka katika hotuba ya kampeni ya uchaguzi 2015* [Unpublished thesis]. Open University of Tanzania.

Rosch, E. (1977). Human categorization. In *Advances in cross-cultural psychology* (Vol. 1). Academic Press.

Saeed, J. I. (2003). *Semantics* (2nd ed.). Blackwell Publishing.

Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili. (2014). *Kamusi ya Kiswahili sanifu* (Toleo la 3). Oxford University Press.

Traugott, E. C., & Dasher, R. B. (2002). *Regularity in semantic change*. Cambridge University Press.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford University Press.